

napa, mikoa wa tanga, Hassan Mkebe, amejitolea kujenga ofisi mbili za chama hicho katika kata hiyo kwa gharama ya Shilingi milioni 22.

Mkebe aliyasema hayo wakati wa aksoma taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM katika Kata ya Nkumba.

Alisema amejenga ofisi ya CCM ya tawi katika Kijiji cha Ubembe, ukumbi wa mikutano na vyumba vya maduka kwa gharama ya shilingi milioni 12.

Alisema baada ya kukamilika ujenzi wa ofisi hiyo, amejenga nyingine ya CCM ya Kata ya Nkumba kwa Shilingi Milioni 10. Mkebe, alisema pia amesaadnia ujenzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo ya sekta ya afya, elimu na maji katika kata hiyo.

Katibu wa CCM Wilaya ya Muheza, Simon Leng'ese, katika sherehe za chama hicho kutimiza miaka 47 zilizofanyika katika kata hiyo, alimpungeza kwa kujenga ofisi hizo mbili za chama.

Aliwataka viongozi wengine wenyewe mapenzi mema kwa chama hicho kuiga mfano huo wa kukisaidia.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Muheza, Laick Gugu, alimpungeza Mwenyekiti huyo kwa kujenga ofisi hizo akisema huo ni utekelezaji wa Ilani ya chama hicho.

Mwenyekiti wa CCM wa Umoja wa Vijana (UVCCM), Aziza Mshakangoto na Jumuiya ya Wazazi, Hatibu Bakari, waliwataka wadau wa chama hicho kuunga mkonon juhudzi za mwenzao huyo wa Nkumba kwa kikipenda kutoka katika damu.



juzi, ambapo Balozi wa Uturuki, Dk. Mehmet Guloglu (hayumo pichani), alishuhudia makabidhiano hayo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

Taasisi zaagizwa kuendeleza 4R

**Na Cynthia Mwilolezi,
ARUSHA**

TAASISI za Serikali zimeagizwa kuendeleza falsafa ya Rais Samia Hassan Suluhu ya 4R kutoa huduma kwa wananchi haraka kupitia Serikali Mtandao (e-GA).

Agizo hilo lilitolewa jana jijini hapa na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete wakati akifunga kikao kazi cha nne cha e-GA.

Ridhiwani aliwasisitiza maofisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kufanya matumizi sahihi ya mitando ili kuharakisha maendeleo kwa serikali na taasisi zake.

Alisema ni lazima e-GA izingatie sheria, viwango na

sera kwa ajili ya ubadilishanaji taarifa za serikali salama. "4R ya Rais wetu ya kuhimiza ustahamiliu siyo kwa wanasiasa pekee bali kila nyanja kwa sababu mageuzi na ujenzi mpya wa maridhiano ni nguzo muhimu katika uletaji chachu ya maendeleo nchini, kuondoa changamoto za wananchi kupitia misfumo inayosomana na naziagiza taasisi za umma kusomana kupitia misfumo ya kidigitali," alisema.

Alisema kuna watu wanatumia barua pepe zisizo rasmi kutapeli wananchi katika ajira na malipo, hivyo wataalamu wa TEHAMA hasa serikali mtandao wanatakiwa kuwa kwa makini ili kuharakikisha usalama wa mitando una-dhibitiwa.

"Kama kuna changamoto ya misfumo kutosomana ni wa-

jibu zizungumzwe kuondoa ukakasi huo na kwenda pamoja katika ujenzi wa kidigitali, ikiwamo maofisa masuhuli kuwajengea uwezo wataalamu wa serikali kufikia malengo ya kidigitali," alisema.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuhakikisha e-GA inafikia malengo na kutoa ufanisi wa kidigitali kupitia misfumo huo.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya e-GA, Benedict Ndomba, alisema miradi ikiwa na misfumo ya TEHAMA, itasaidia kuokoa fedha za umma na za serikali.

"Tunamshukuru Rais Samia Hassan Suluhu kwa kujenga serikali kidigitali, lakin naomba Serikali kuweka mazingira wezeshi kwa e-GA katika kuleta ufanisi zaidi,"

alisema.

Mkurugenzi wa e-GA Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Said Seif Said, alipongeza ushirikiano baina Zanzibar na Tanzania Bara kwa ajili ya kuhakikisha utendaji kazi ofisini unakuwa kwa kasi kupitia teknolojia hizo. Akisoma maazimio yaliyofikiwa kwenye kikao kazi hicho, Priscas Kiwango kuwa ni pamoja na kila taasisi kuteua ofisa TEHAMA kusimamia miongozo na kanuni za usimamizi bora wa mtandao, taasisi za umma ziboreshe na kutumia teknolojia hiyo.

Nyingine ni utoaji huduma kwa wananchi, kufanya tathmini ya hali ya TEHAMA, uundaji wa ripoti katika kila taasisi husika na kuwasilisha e-GA kabla ya mwaka wa fedha.